Bw. Marshall D. Orson, Mwenyekiti wa Bodi
Bi. Vickie B. Turner, Mwenyekiti Msaidizi
Bw. Stan O. Jester
Dkt. Michael A. Erwin
Bi. Allyson Gevertz
Bw. Diijon DaCosta
Dkt. Joyce Morley

Bi. Cheryl Watson-Harris, Msimamizi wa Muda

INAPASWA KUTANGAZWA MARA MOJA

Julai 14, 2020

Anwani:
Portia Kirkland, 678-427-4898
Carla Parker, 404-734-1717

Mpango wa Kufungua Upya wa DCSD: Kucheleweshe Kuanzishwa kwa Mwaka wa Masomo, kwa kutumia Mfumo wa Kusoma kwa Mbali

STONE MOUNTAIN, Ga. – Msimamizi wa Wilaya ya Shule za Jimbo la DeKalb, Cheryl Watson-Harris aliwasilisha mpango wa kufungua upya shule wa Wilaya wakati wa mkutano wa jana wa Halmashauri ya Elimu.

Mpango wa sasa unapendekeza kwamba halmashauri ya shule icheleweshe kuanzishwa kwa mwaka wa masomo wa 2020-2021 hadi Agosti 17, 2020, na ifungue shule kwa kutumia mfumo wa kusoma kwa mbali ili kupunguza kuenea kwa COVID-19. Halmashauri imeidhinisha tarehe ya kucheleweshe kuanzishwa kwa mwaka wa masomo.

Tathmini zilizosasishwa na marekebisho ya mpango zitashirikiwa kila mwezi.

Mpango wa Wilaya umejumuisha mwongozo wa sasa kutoka kwa Idara ya Afya ya Umma ya Georgia, Halmshauri ya Afya ya Kaunti ya DeKalb, Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDS), Idara ya Elimu ya Georgia (GaDOE), Shirika la Huduma ya Elimu Mjini (MRESA) kwa kushirikiana na wasimamizi, na maafisi wa ndani na wa serikali. Maoni ya jamii kutoka kwa utafiti wa mchango wa washikadau, ambao ulizalisha majibu 39,574 kutoka kwa wazazi, wanafunzi na wafanyakazi, yalisaidia pia katika kuunda mpango huu.

“Usalama wa wanafunzi na wafanyakazi wetu ndio kipaumbele cha Wilaya ya Shule za Jimbo la DeKalb, na kwa wakati huu tunapendekeza mfumo wa kusoma kwa mbali uanzishe mwaka huu,” alisema Msimamizi Cheryl Watson-Harris. “Kwa kuzingatia kiwango wastani cha kuenea kwa magonjwa kwa sasa katika eneo letu, chaguo hili ndilo chaguo letu bora, lakini litathminiwa upya mara kwa mara. Wanafunzi, walimu na wafanyakazi watakuwa pia wakipokea rasilimali zaidi za kuwasaidia katika mazingira ya mbali.”

Wilaya inanunua Chromebooks za 1:1 ili kuhakikisha wanafunzi katika gredi za Pre-K hadi 12 wanapata kifaa. Wanafunzi na wazazi wataweza kuona masomo ili kujifunza jinsi ya kutumia vizuri rasilimali za programu, pamoja na, lakini haijakomea kwa VERGE na Microsoft TEAMS.

DCSD pia itatoa ufikiaji wa VERGE na Microsoft TEAMS kwa washauri wa shule ili kutekeleza vikao vya mwongozo, na hata pia kuendelea kutoa Mafunzo ya Youth Mental Health First Aid 101 kwa wafanyakazi. Shule na walimu wamewezeshwa kuchagua zana mbadala kama vile Zoom na Darasa la Google (Google Classroom) na wataendelea kuelezea rasilimali zinazofaa kwa wanafunzi na wazazi wao.

Kuanzia Julai 14, kwa miezi 12 wafanyakazi wataanza kutumia njia tofauti, ili kuandaa shule kufunguliwa. DCSD inatengeneza ratiba tofauti ambazo zitawaruhusu walimu, wahudumu wa msaada, na wafanyakazi kufikiria kwa usalama rasilimali za masomo na/au kukagua vifaa ili kujiandaa kwa mwanzo wa mwaka wa shule.

DCSD pia inaunda nyenzo za maendeleo ya kitaaluma ili kuwaunga mkono walimu na viongozi, ikiwa ni pamoja na kuhusu kiwewe, ubaguzi, mafunzo ya kijamii-kihisia, jumuisho na matumizi yanayofaa ya zana na mifumo ya mafunzo ya kidijitali na mtandaoni. Vikao vya maendeleo ya kitaaluma vitatolewa ili kushiriki kanuni na mikakati bora ya kufunza na kufuatilia maendeleo ya wanafunzi vizuri katika mazingira ya kusoma kwa mbali.

Walimu watakuwa na nafasi ya kushiriki katika masomo landanishi ambayo yanalenga jinsi ya kutumia Microsoft Teams na Zoom ili kuwezesha masomo ya moja kwa moja, kukuza kuhusika kwa wanafunzi, na kutoa misaada lengwa kupitia mikutano ya video.

Wilaya inapanga vyakula mbalimbali, ambavyo vinatimiza maelekezo ya serikali kwa kila kiwango cha gredi, kwa kiamsha kinywa, chakula cha mchana, na vitafunio (kama inavyotumika). Idara ya Lishe itashirikiana na Idara ya Usafiri ili kutoa vyakula kwenye njia za basi kwa familia ambazo haziwezi kufikia usafiri.

Mpango huu unataka mfumo wa masomo ulingane na mpango husika wa kudhibiti kuenea kwa magonjwa katika jamii. Ikiwa magonjwa yanaenea kidogo au hata hayaenei, basi mfumo wa kawaida utatumika. Ikiwa magonjwa yanaenea kidogo au wastani, aidha masomo ya kawaida, tofauti au ya mbali yatatumika. Kwa sasa, magonjwa katika eneo hili yanaenea kwa kiwango wastani, kwa hivyo mfumo wa kusoma kwa mbali unapendekezwa.

Wilaya itaendelea kufuatilia data ya sasa ya COVID-19 na kutathmini kiwango cha kuenea ili kubainisha ni lini mfumo wa sasa wa masomo unapaswa kurekebishwa. Tathmini itawasilishwa wakati wa mikutano ya halmashauri mnamo Sept. 14, Okt. 19, Nov. 9, na Des. 7, 2020.

Utafiti wa mchango wa jamii ulionyesha kwamba wafanyakazi wengi (asilimia 70) na wazazi (asilimia 59) hawako sawa na mfumo wa kawaida wa masomo kuwa wa kuanzisha mwaka. Mifumo tofauti na mifumo ya mbali ilipendelewa zaidi katika vikundi vyote. Wanafunzi waliashiria kupendelea mfumo wa kawaida.

Bofya hapa ili kupitia uwasilishaji wote wa https://www.dekalbschoolsga.org/documents/plan-presentation.pdf , ikiwa ni pamoja na maelezo kuhusu itifaki zilizosasishwa za usafishaji na matengenezo.